HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
KAZI ZA NYUMBANI **AWAMU YA KWANZA** APRIL 2020
MAAFIFA YA JAMII DARASA LA VII
**KAZI YA KWANZA**

**SEHEMU A: URAIA**

Chagua jibu lililo sahihi zaidi kwa kuweka kivuli herufi ya jibu sahihi kwenye karatasi ya kujibia uliyopatiwa.

1. Jukumu la ulinzi na usalama katika kata ni la___________
   (a) kamati ya maendeleo ya kata (b) baraza la mila la kata (c) serikali kuu
   (d) halmashauri ya maendeleo ya Wilaya (e) wanajamii wote katika Kata.
2. Sentensi ipi ni sahihi kuhusiana na mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya
   (a) Huchaguliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri (b) Huchaguliwa na baraza la madiwani la wilaya (c)Huchaguliwa na Wabunge (d) Hudumu kwa miaka 10 baada ya kuchaguliwa (e)Huteuliwa na Waziri wa Serikali za Mitaa
3. Chombo kinachohusika na kutoa hukumu ya makosa ya jinai ni________
   (a) Jeshi la polisi (b) Mahakama (c) Magereza (d).Idara ya uhamiaji (e). Jeshi la wananchi
4. Mambo ambayo kila binadamu anastahili kuyapata bila kujali kabila, utaifa au jinsia huitwa
   (a)Utawala bora (b)Utawala wa sheria (c) demokrasia (d) haki za binadamu
   (e) mbunge wa viti maalumu
5. Mashirika yafuatayo ni ya kimataifa isipokuwa______________
   (a) WHO na UNICEF (b)FAO na ILO (c) UNDP na UNHCR (d) UNDP na UNESCO
   ( e) TANESCO na NDC
6. Kwa mujibu wa katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania, mgombea wa nafasi ya Urais anapaswa kuwa na miaka kuanzia:-________________
   (a) 21 na kuendelea (b) 61 na kuendelea (c) 50 na kuendelea (d) 40 na kuendelea
   (e) 18 na kuendelea
7. Sentensi ipi sio sahihi kuhusiana na mwalimu Julius K.Nyerere_______________
   (a) Alikuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika (b) Alikuwa Rais wa kwanza wa Tanzania
   ( c) Alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika (d) Alikuwa waziri Mkuu wa kwanza wa Tanzania (e) Alifariki tarehe 14.10.1999
8. Uchaguzi wa kwanza ulioshirikisha vyama vingi nchini Tanzania ulikuwa mwaka_______________
   (a) 1995 (b) 1992 (c) 2005 (d) 2010 (e) 2000.
9. __________ ni kiongozi wa shughuli zote za serikali Bungeni
   (a) Rais (b) Waziri Mkuu (c ) Spika wa Bunge (d) Mwanasheria Mkuu ( e) Makamu wa Rais
10. Mojawapo ya changamoto wanazozipata wajasiriamali ni pamoja na ______________;
    (a) Ukosefu wa leseni za biashara (b) Kutokuwepo kwa benki na taasisi za fedha (c) Upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma (d) Uwepo wa askari polisi na mgambo wengi maeneo ya mjini (e ) Kutokuwepo kwa sera ya uwekezaji
11. Jaji mkuu huteuliwa na __________
    (a) Rais (b) Waziri mkuu (c) Bunge (d) Makamu wa Rais (e) Mwanasheria Mkuu

12. Ili kudumisha amani na umoja wa Kitaifa tunapaswa__________
    (a) Kuenzi lugha za makabila (b) Kutii sheria bila shuruti (c) Kuenzi umoja wa makabila yetu (d) Kuhakikisha kila raia wa Tanzania anaenda shule na kupata (e)Kila raia apitie mafunzo ya Kijeshi
13. Kwa mara ya mwisho Tanzania ilifanya sensa mwaka gani?
    (a) 2012 (b) 2009 (c) 2002 (d) 2013 (e) 2010

14. Mwakilishi wa wananchi katika vikao vya wilaya vya serikali za mitaa ni____________
(a) Mkuu wa wilaya (b) Mwenyekiti wa serikali za vijiji (c) Afisa mtendaji kata (d) Mwenyekiti wa wilaya wa chama tawala (e) Diwani wa kata

**SEHEMU B: HISTORIA**

15. Zifuatazo ni hatua muhimu za kiuchumi katika mifumo ya maendeleo ya uzalishaji mali _________
(a) Ujima, Ukabaila, utumwa, ubepari na ujamaa (b) Ujima, ubepari, ujamaa , utumwa, na ukabaila
(c)Ujamaa, Ujima, utumwa, ubepari na ukabaila (d) Ujima, ubepari, utumwa, ujamaa na ukabaila
(e) ubepari Ujima, ukabaila, utumwa, na ujamaa

16. Serikali ya Kijerumani ilitawalaje Tanganyika?
(a) Utawala wa moja kwa moja (b) Utawala usio wa moja kwa moja (c) Uwagawe na uwatawale (d) Kuwatumia viongozi wa jadi na machifu (e )Kutumia mtutu wa bunduki

17. Kinjekitile Ngwale aliwaagiza wafuasi wake kutumia maji maalumu aliyoyaandaa wakati wa vita vya majimaji akiwa na lengo la __________.
(a) Kuwatia moyo Waafrika katika mapambano na Wajerumani (b) Kuonyesha nguvu ya uchawi wake (c) Kutumia sayansi ya Kiafrika katika vita (d) Kubadili risasi kuwa maji (e)Kuwachanganya.

18. Wazungu walitumia mbinu ipi kati ya zifuatazo kuanzisha ukoloni barani Afrika?
(a) Kuweka mikataba ya ulaghai na viongozi wa jadi (b) Kutoa misaada ya nguo na chakula ( c) Kuwachukua watu utumwani (d ) Kuwapatia wananchi huduma za kijamii
(e ) Kufanya biashara za kubadilishana

19. Mwanadamu wa mwazo aliyeanza kutembea kwa miguu miwili alijulikana kama _____________
(a). Primates ( b) . Homo sapiens (c) Homo Habilis (d) Zijnjanthropus (e) HomoErectus

20. Jamii za Afrika Mashariki zilizowapinga wakoloni kwa njia ya vita ni pamoja na
(a) Wanandi na Wahehe (b) Wasangu na Wabena (c) Waha na Wakamba (d )Waganda na Wabena ( e) Wabena na Wapare

21. Umoja wa mataifa (UNO) ni chombo kilichoundwa baada ya vita kuu ya pili ya dunia ambavyo vilikuwa mwaka ______________
(a) 1914 – 1918 ( b) 1884 – 1885 ( c) 1905 – 1907 (d) 1978 – 1979 (e) 1939 – 1945

22. Chombo kilichoundwa kutokana na nchi zilizotawaliwa na waingereza kiliitwa ____________
(a) Jumuiya ya Madola (b) ECOWAS (c) COMESA (d) UN ( e ) EAC

23. ________ni vyama vya siasa vilivyopigania Uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.
(a) TANU na ASP (b) TAA na UTP (c) UTP na ZPPP (d) ANC na ASP (e ) TANU na SHIRAZ

24. Mwanasayansi aliyesoma na kutafiti mabadiliko ya mwanadamu na kujumuisha kuwa kiumbe huyo yupo kwenye kundi la Sokwe watembeao kwa miguu minne, anajualikana kwa jina la___________
(a) Charles Leakey ( b) Dr. Leakey (c) Charles dorwin
(d) Livingstone na Dr. Leakey ( e) Rebman na Dr. Leakey

25. Vita vya kikabila vilivyosabisha wangoni kuhama nchini Afrika Kusini vinajulikana kwa jina la_________
(a) Mfekane (b) Msafara wa Makaburu (c ) Maji maji (d) Khoisan
(b) Vita baridi

26. Mabadiliko ya mwanadamu kutokea mfumo mmoja kwenda mwingine hujulikana kama _______
(a) Uumbaji ( b) Mapinduzi (c) Maendeleo (d ) Mageuzi ( e) Teknoloji

27. Moja kati ya mbinu zifuatazo ilitumiwa na watawala wa kikoloni kudhoofisha ama kuua kabisa teknolojia ya Waafrika ______________

(a) Kubinafsisha viwanda vya Kiafrika (b) Kufundisha kusoma na kuandika (c) Kufundisha Waafrika teknolojia za Ulaya (d) Vita vya mara kwa mara (e) Kuchoma viwanda vya waafrika

28. Katika hatua za mwanzo za maendeleo ya ukuaji wa uchumi, Ugunduzi wa moto ulimsaidiaje binadamu? ___________

(a) Kujikinga na baridi, kuimarisha zana za mawe na kujihami (b) Kujikinga na baridi, kutengeneza chakula, kujihami na wanyama wakali na kuwinda (c) Kujikinga na wanyama wakali, kujenga nyumba bora na kulima (d) Kijikinga na baridi, kujenga nyumba, na kufuga wanyama (e) Kufuga wanyama, kujikinga na baridi, kujenga nyumba bora, na kupika

29. Ulimaji wa mazao ya biashara wakati wa utawala wa kikoloni ulisababisha uhaba wa chakula katika jamii za kiafrika kwa sababu_________

(a) Waafrika walitamani kulima kilimo biashara (b) Waafika waliona mazao ya biashara yana faida zaidi (c) Waafrika walilazimishwa kupanda mazao ya biashara zaidi ya mazao ya chakula (d) Waafrika walikosa mbegu za mazao ya chakula ( e) Mazao ya biashara yalikuwa na soko kwa wafrika

30. Ngome ya yesu ilijengwa Mombasa nchini Kenya na______

(a) Waingereza (b) Wareno (c) Wajerumani (d) Wahispania (e ) Waarabu

**SEHEMU C: JIOGRAFIA: Chagua jibu sahihi na weka kivuli kwenye herufi ya jibu sahihi**

31. Zifuatazo ni faida zitokanazo na madini katika uchumi isipokuwa_________

(a) Kutupatia fedha za kigeni (b) Kutoa ajira (c) Kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda (d) Ufyekaji wa misitu kwa ajili ya uchimbaji wa madini ( e) Husaidia ukuaji wa miji katika maeneo ya uchimbaji

32. Kwa nini tunashauriwa kubadilisha upandaji wa mazao katika shamba _______

(a) Kuzuia wadudu waharibifu na kurutubisha udongo (b) Kuzuia mmomonyoko wa udongo (c )Kuzuia uharibifu wa misitu (d) Kuzuia uchafuzi wa hewa (e) Kuzuia uchafuzi wa maji

33. Nchi za Afrika mashariki zipo katika uwanda wa kitropiki lakini hali ya hewa tofauti. Hii ni kwa sababu ya ________ (a) Kuwepo kwa nyanda tofauti za hali ya hewa (b) Kuwepo kwa aina tofauti za milima (c) Kukosekana kwa mito ya kutosha (d) Kuwepo kwa tofauti za mipaka (a) Kuwepo kwa uongozi tofauti kwa kila nchi.

34. Umbo lifuatalo ni matokeo ya __________



(a) nguvu ya mvutano (b) Nguvu ya mgandamizo (c )Nguvu ya volkano (d) Nguvu ya mlipuko (e ) Nguvu ya mvutano na volkano

35. Moja ya madhara ya kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu nchini Tanzania ni__________

(a) Kuongezeka kwa vita vya kikabila (b) kuongezeka kwa ugonjwa wa malaria (c) Kukosa huduma toshelevu za kijamii (d) kupungua kwa eneo la nchi (e) kutopata idadi ya wasomi wa kutosha

36. Ikiwa ni saa 5.30 Asubuhi katika mji wa Lilongwe nyuzi 34 Mashariki, je itakuwa ni saa ngapi katika mji wa Mogadishu uliopo nyuzi 45 Mashariki ?___________

(a) Saa 5:44 asubuhi (b) Saa 4:16 asubuhi (c ) Saa 6:14 Mchana (d) Saa 4:16 usiku (e )Saa 5.30 asubuhi

37. Mistari ya kubuni inayochorwa kwenye ramani kutoka kaskazini kwenda Kusini uitwaje? -----------

(a) Longitude (b) Ikweta (c). Kizio cha aktiki (d) .Latitude (e ) Griniwichi

38. __________ni uoto wa asili unaopatikana mwambao wa bahari ya Hindi nchini Tanzania

(a) Ukanda wa kisavana (b) Vichaka (c ) Ukanda wa kitropiki (d) Misitu ya mikoko (e) Ukanda wa nyasi

39. Chombo kitumikacho kupima kiwango cha unyevunyevu kwenye hewa kinajulikana kwa jina la___________

(a) Windvane (b) Hydrometa (c ) Rain geji (d) Barometa (e )Hygrometa

40. .Nchi za mashariki ya kati ni maarufu kwa uzalishaji wa _________

(a) Mafuta (b) korosho (c ) Miwa ( d) Dhahabu ( e) Ndizi

41. Sehemu ya jangwa ambayo maji hupatikana huitwa_______

(a) Chemchem ( b) Visiwa (c ) Oasisi (d) Mto (e ) Kreta


42. Jua la utosi katika mwezi Disemba huwa katika ____________

(a) Kizio cha Kusini (b) Tropiki ya Kansa (c) Ikweta (d) Kizio cha Kaskazini (e) Tropiki ya Kaprikoni

43. Kupwa na kujaa kwa maji baharini kunasababishwa na tukio lipi? ________

(a) Dunia kuzunguka jua (b) Mvutano kati ya Dunia na Mwezi (c) Dunia kujizungusha kwenye mhimili wake (d) kupatwa kwa jua (e ) Kupatwa kwa Dunia

**Soma kielelezo hapo chini kisha jibu maswali yafuatayo :-**




44. Herufi **B** inawakilisha ____

(a) Pitio (b) Njia (c ) Mto (d) Mfereji (e )Daraja

45. Tofauti kati ya kontua moja na nyingine ni _____

(a) m. 100 (b) m.150 (c ) m.400 (d) m.0 (e ) m. 250